## Kwa Ufupi

# Wakulima, wafugaji wazuia msafara wa Waziri Ulega

**Kiteto.** Kutokana na madai ya kukiukwa kwa makubaliano ya wananchi wa vijiji vya Partimbo, Njoro, Ndaleta wilayani Kiteto Mkoa wa Manyara na Wakala wa Misitu Tanzania (TFS), baadhi ya wakulima na wafugaji wamelazimika kusimamisha msafara wa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Andallah Ulega wakitaka asuluhishwe.

Wananchi wamedai kutumia eneo linalolalamikiwa kwa zaidi ya miaka 15, huku TFS nayo ikija na mpango wa kulihifadhi eneo hilo.

Wakiwa wameshika majani kama ishara ya amani, wananchi hao walimsimamisha Naibu Waziri huyo na aliposimama walidai baadhi yao wamekamatwa na vyombo vya dola kwa kukutwa eneo hilo.

Hali hii ikamlazimu Naibu Waziri Ulega kumpigia simu Meneja wa TFS, Profesa Dos Santos Silayo mbele ya wakulima na wafugaji. na kumweleza kilio hicho cha wananchi

Akizungumza kwa njia ya simu huku wananchi hao wakisiliza, Profesa Silayo aliwaahidi atakwenda kulishughulikia suala hilo akisema yuko katika makabidhiano ya ofisi. "Mkuu wa wilaya nakuagiza shughulikia migogoro hii fuatilia tupate majibu ya wafugaji tisa waliokamatwa ambao dhamana yao nimeambiwa imefungwa, watu hawa wasibughudhiwe mpaka majibu haya yatakapopatikana," alisema Naibu Waziri Ulega. **(Mohamed Hamad)**

CamScanner

# Samia atimiza ndoto ya Nyerere Bwawa la Kiteto

Na Mwandishi Maalumu

RAIS Dk Samia Suluhu Hassan ametimiza ndoto ya Rais wa Serikali ya Awamu ya Kwanza, Julius Nyerere kwa kujenga upya bwawa ambalo Baba wa Taifa alilijenga mwaka 1975 na likapasuka mwaka 1978.

Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega alisema hayo mwishoni mwa wiki alipofanya ziara ya kikazi katika Wilaya ya Kiteto mkoani Manyara kukagua bwawa la Kaiwang katika Kijiji cha Ndedo.

Ujenzi wa bwawa hilo ukikamilika maji yatatumiwa na mifugo, wanyama wa porini na matumizi ya binadamu.

Ulega alisema ni fahari kwa Rais Samia kutimiza ndoto ya Nyerere kwa kuzingatia maono yake kwa kuhakikisha bwawa hilo linaanza kufanya kazi upya na akasema mkandarasi amelifanyia tafiti na muda wowote kuanzia sasa ataanza kufanya kazi ya ujenzi.

"Rais Samia Suluhu Hassan anakuja kutimiza ndoto ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Anafanya mengi yaliyootwa na kuwazwa na Rais wa Awamu ya Kwanza hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na tayari fedha zimetengwa," alisema.

Wakazi wa Wilaya ya Kiteto wameomba bwawa hilo liitwe Mama Samia Kaiwang kwa kushukuru jitihada zinazofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita.

Ulega aliagiza wananchi hao walitunze liwe na tija kwao kwa kuwa watapata maji mengi na kuondokana na adha hiyo kwa mifugo.

Mbunge wa Jimbo la Kiteto, Edward Ole Lekaita alisema mradi huo utawawezesha wananchi wa eneo hilo kumkumbuka Rais Samia maisha yao yote kwa kuwa asilimia 90 ya wakazi wanaozunguka bwawa hilo ni wafugaji.

Ole Lekaita alisema wanashukuru namna Serikali ya Awamu ya Sita inavyoshughulika na changamoto zinazowakumba wananchi wakiwemo wafugaji hasa katika suala la mabwawa, malisho na majosho.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto, John Nchimbi alisema eneo la kujenga bwawa hilo lifanyiwa tafiti ukiwemo wa miundombinu na uimara wa udongo na akasema wanatarajia ujenzi wa bwawa hilo utagharimu zaidi ya shilingi milioni 500.

CamScanner

# kufugia kuku

Na Amina Omari, Tanga

MKUU wa Mkoa wa Tanga, Omari Mgumba ametaka wananchi mkoani humo kuacha tabia ya kubadili matumizi ya vyandarua vya msaada vinavyotolewa na serikali katika jitihada za kupambana na ugonjwa wa malaria kwa kufugia kuku au kuvulia samaki.

Mgumba alitoa onyo hilo wakati wa uzinduzi wa ugawaji wa vyandarua kwa wanafunzi wa shule za msingi mkoani Tanga ambapo shule zote 1,083 katika wilaya zote nane zitafikiwa.

"Napenda kuwaagiza viongozi wote wa serikali, dini na jamii kusimamia matumizi sahihi ya vyandarua hivi, jamii ielimishwe umuhimu na matumizi sahihi ili kuepuka matumizi yasiyotarajiwa," alisema.

Mgumba alibainisha kwamba ili kuhakikisha kiwango cha maambukizi ya malaria kinapungua hadi kufikia asilimia 0 ifikapo mwaka 2030, serikali imeandaa ugawaji wa vyandarua vyenye viuatilifu kwa wanafunzi hao kuanzia darasa la kwanza hadi la saba.

Meneja wa Bohari ya Dawa (MSD) Mkoa wa Tanga, Siti Abdulrahman alisema serikali imewapa jukumu la kusambaza vyandarua hivyo kwa mikoa ya Iringa, Dodoma, Manyara, Kilimanjaro na Tanga.

CamScanner

# RC awatangazia 'vita' wanaotumia vyandarua kufugia kuku, samaki

**Na Hamida Kamchalla,**
TANGA

MKUU wa Mkoa wa Tanga, Omari Mgumba, amewanyooshea 'kidole' wananchi wanaotumia vibaya vyandarua vya msaada vinavyotolewa kwa ajili ya kujikinga na maambukizi ya ugonjwa wa malaria.

Amezionya baadhi ya familia zinazotumia vyandarua hivyo, kama nyumba za kufugia kuku na miundombinu ya kuvulia samaki katika Bahari ya Hindi na mabwawa.

Alitoa onyo hilo jana jijini Tanga, wakati wa uzinduzi wa ugawaji wa vyandarua kwa wanafunzi wa shule za msingi 1,083 zilizoko mkoani humo.

"Nawaagiza viongozi wote wa serikali, dini na jamii, kusimamia matumizi sahihi ya vyandarua hivi.

Jamii ielimishwe umuhimu na matumizi sahihi ili kuepuka matumizi yasiyotarajiwa, kama tulivyoshuhudia kwenye mipango mingine iliyopita.

"Walimu shuleni kwa kushirikiana na wataalamu wa afya, mtoe elimu na kusisitiza matumizi sahihi ya vyandarua hivi, kwa wanafunzi wakati wa ugawaji shuleni," alisisitiza Mgumba.

Alisema ili kuhakikisha kiwango cha maambukizi ya malaria kinapungua hadi kufikia asilimia sifuri ifikapo mwaka 2030, serikali kupitia Wizara ya Afya na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), imeandaa mpango wa ugawaji wa vyandarua vyenye viuatilifu kwa wanafunzi hao kuanzia darasa la kwanza hadi la saba.

Katika hafla hiyo, Meneja wa Bohari Kuu ya Dawa (MSD), Mkoa wa Tanga, Siti Abdulrahman, alisema kuwa serikali imewapa jukumu la kusambaza vyandarua hivyo kwa mikoa ya Iringa, Dodoma, Manyara, Kilimanjaro na Tanga.

Alisema kwa Mkoa wa Tanga wamepatiwa vyandarua 529,641 vya Sh. bilioni 2.6 vitakavyogawiwa kwa shule zote za msingi kuanzia mwanafunzi wa darasa la kwanza hadi la saba.

Mkuu wa Wilaya ya Tanga, Hashimu Mgandilwa, alisema kwa nafasi yake ana uwezo wa kuingia mahali popote akishirikiana na viongozi wengine wa serikali kuhakikisha wananchi hawaendi kinyume na matakwa yaliyowekwa.

CamScanner